

## Unyanyazaji wa kinyumbani ni nini?

Unyanyasaji wa kinyumbani ni wakati mshiriki, mwenzi, mpenzi, au mwanafamilia mwingine wa familia yako au familia anasema au anafanya kitu cha kukufanya uhisi hofu au kukudhibiti.

Unyanyasaji unaweza kuwa wa kimwili, kimapenzi, kihemko au kiuchumi.

Mifanyo mingine ni:

- Kugonga, kuchapa au kusukuma
- Kukuzuia kupata au kuhifadhi ajira
- Kudhibiti ufikiaji wako kwa pesa
- Kukuzuia kupigia simu au kuona familia yako au marafiki
- Kukushusha, kukuita majina yasiyostahili, au kukuaibisha
- Kukufuata au kukuzuia kuteamba kwa uhuru
- Kukutishia kukuumiza, watoto wako, au kipenzi chako



**Kwa usaidizi, pigia:  
National Coalition Against  
Domestic Violence Hotline  
1-800-799-7233**

**Au tembelea  
[www.endabusewi.org](http://www.endabusewi.org).**

Kuna watu katika jamii yako ambao wanaweza kukusaidia na:

- Ushauri wa mgogoro
- Upangaji wa Usalama
  - Kutafuta makazi
  - Vikundi vya msaada
  - Uwakikishaji na polisi
- Rufaa kwa sheria na huduma zingine

**Habari ya Anwani ya Shirika la Karibu  
la Unyanyasaji wa Kinyumbani**

Department of Children and Families ni mwajiri wa fursa sawa na mtoaji huduma. Ikiwa una ulemavu na unahitaji kufikia huduma, pokea habari katika muundo mbadala, au unahitaji habari kutafsiriwa katika lugha nyingine, tafadhali pigia kwa 608-535-3665. Watu ambao ni viziwi, ugumu ya kusikia, viziwi-kipofu au walemavu wa usemi wanaweza kutumia Wisconsin Relay Service (WRS) – 711 bure kuwasiliana na idara.


[f @WisDCF](https://www.facebook.com/WisDCF) [@WisDCF](https://www.instagram.com/WisDCF) [dcf.wisconsin.gov](http://dcf.wisconsin.gov)

DCF-P-2614-SW (R. 11/2021) (T. 12/2021)

## Kukumbwa na Unyanyasaji wa Kinyumbani

**Jinsi Ya Kukusaidia**

FACING DOMESTIC VIOLENCE -  
HOW W-2 CAN HELP YOU



Wisconsin Department of  
Children and Families



## Tunaweza saidia vipi?

Ikiwa unyanyasaji wa kinyumbani ni tatizo kwako, ongea na mfanyakazi wako wa W-2. Shughuli zako zingine za W-2 zinaweza kubadilishwa wakati unashughulika na unyanyasaji wa kinyumbani.

### Kazi

Kwa muda mfupi, huenda usifanye utafutaji wa ajira na/au shughuli za uzoefu wa kazi ikiwa unafanya shughuli hizi:

- Inakuweka wewe au watoto wako katika hatari ya unyanyasaji wa kinyumbani, au
- Inufanya iwe ngumu kwako kuondokea unyanyasaji wa kinyumbani.

## Vipimo vya Muda

Katika kipimo cha kupata ni miezi 48. Unaweza kupata kwa zaidi ya miezi 48 ikiwa kupoteza yako kuta:

- Kuweka wewe au watoto wako katika hatari ya unyanyasaji wa kinyumbani, au
- Kuifanya iwe vigumu kwako kuondokea unyanyasaji wa kinyumbani.

## Msaada wa Mtoto

Unaweza kosa kushirikiana na Msaada wa Watoto ikiwa ita:

- Fanya iwe ngumu zaidi kwako au mtoto wako kuondokea unyanyasaji wa kinyumbani; au
- Inaweza kukuweka wewe au mtoto wako hatarini.

Kushirikiana kunamaanisha kutoa habari kwa Msaada wa Watoto ili waweze kutoa malipo ya msaada wa Watoto kwa mtoto wako. Ikiwa unashirikiana na Msaada wa Watoto, unaweza kuwaomba kuweka anwani yako na nambari ya simu siri.

## Unaweza kumwambia mfanyakazi wako wa W-2 kuhusu unyanyasaji wa kinyumbani wakati wowote.

Ukiamua kumwambia mfanyakazi wako kuhusu unyanyasaji wa kinyumbani, shughuli zinaweza kuwekwa katika mpango wako wa Ajira ambao husaidia kukuweka wewe na watoto wako salama.

Mifano mingine ni:

- Kwenda mikutano ya ushauri na msaada
- Kutafuta pahali salama pa kuishi
- Kupata msaada wa kisheria na uwakilishaji
- Kufanya mipango ya usalama na mawakili wa unyanyasaji wa kinyumbani

**Chochote unachomwambia mfanyakazi wako kuhusu unyanyasaji wa kinyumbani ni cha faragha. Laikini, ukimwambia mfanyakazi wako kuwa watoto wowote wananyanyaswa, mfanyakazi wako lazima aripoti habari kwa huduma za kinga za watoto.**

